

Karibu ABA



Academia ya Bright Africans (ABA) ni mradi wa shule uliojitokeza kutokana na maono aliyekuwa naye Mariam Sambe tangia ujana wake. Mnamo mwaka wa elfu mbili na sita (2006) alianza kulitia mkazo wazo hili. Alilenga mfumo wa elimu wa kiumla; lenye lengo la kuchangia katika maendeleo endelevu barani Afrika, kuanzia na Uhabeshi (Ethiopia). Mariam alitamani kutengeneza mpangilio ambalo lingeweza jamii kujihusisha na shughuli za kustahimili ustawi wa kijamii na uchumi. Hamna njia bora yakutimiza hayo ila kuzindua mfumo wa elimu uliyo kamilifu na inayoweza watoto, waalimu, wafanyakazi na wazazi kufanya kazi kwenye mazingira ya heshima na manufaa. Hili ndilo nguzo la ABA!

Elimu katika ABA utawekwa kwenye msingi wa Elimu wa kiumla, “Filosofia ya elimu iliyo na msingi wake kwenye nguzo kwamba kila mtu hupata utambulisho, maana na kusudi maishani kwa njia ya uhusiano na jamii, uhusiano na mazingira asili, na katika maadili ya kibinadamu kama vile huruma na amani” (Miller, 1997). Kwa vingine, ni lazima wanafunzi wawe na uhusiano na mazingira asili, jamii, na maadili ya uhisani ndiposa wawe na subira maishani. Kujifunza heshima, huruma, na amani lazima iambatane na mafanikio ya kitaaluma. Elimu ya kiumla yaweza hayo kutokea. Jean-Jacques Rousseau alikuwa miongoni mwa wanafilosofia na wakufunzi wa kwanza ambao waliangazia maendeleo ya binafsi ya binadamu kwa kikamilifu. Aliamini kwamba watoto wanafaa kusomeshwa kwa kuzingatia muktadha wa mahali wanamoishi, kitongoji na pia familia. Watoto hujifunza kutokana ma mazingira yao, hivyo basi kuzingatia hiyo ni muhimu kwa maendeleo yao (Miller, 2007).

Mmoja wa viongozi wa harakati wa elimu ya kiumla, Ron Miller (1992), anasema kwamba elimu ya kiumla haifai kuzingatiwa kama mbinu maalum ambayo haiwezi badilika. Ni dhana inayofaa kutumika kwa kuzingatia tamaduni na mahitaji ya wanafunzi. Hivyo basi ABA itabuni mpango wa elimu ya kiumla ambayo itaambatana na tamaduni na mahitaji ya watoto watakao jiunga na shule hili.